

HABARI LEO WK 5.

# Vijana 440 waingizwa BBT kunenepesha, kuuza ng'ombe

Na Magnus Mahenge,  
Dodoma


**Z**AIDI ya Vijana 440 wameingizwa kwenye Mpango wa Kujenga Kesho iliyobora zaidi (BBT) kwa kununua ng'ombe minadani, kunenepesha na kuuza kwenye viwanda vya kuchataka kwa faida na tija.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulenga alisema hayo jijini hapa wakati akizungunza na vyombo vya habari kwamba mkakati huo wa wizara unalenga kusaidia vijana katika maeneo ambayo kuna viwanda vya kuchakata mifugo na mifugo mingi.

"Katika mkakati huo wa wizara tumeanza na vijana

240 ambao wapo katika sekta ya mifugo ambao hadi Agosti mwaka huu, tayari wamepata faida ya shilingi milioni 74 kutokana na kununua ng'ombe minadani,

**Mikoa mingine ya Arusha na Pwani imechaguliwa kuanza mpango huo kutokana kuwa na viwanda vingi hasa vya kuzalisha na kuchakata mifugo.**



kisha kuwanepesha na kuwauza kwenye viwanda vya kuchakata," alisema.

Ulega alisema, katika kampeni hiyo ya uboreshaji mifugo, vijana hao wamefaulu kunenepesha ng'ombe walionunua minadani kwa miezi mitatu na kisha kuwauza baada ya kuwanepesha viwandani kwa faida.

Vijana hao wanaotoka katika kada mbalimbali za wasomi na wasio wasomi, wameingizwa katika mpango huo wa kunenepesha mifugo, kuuza kwenye viwanda lengo ni kutumia fursa ya uwepo wa viwanda, kupata ajira na faida.

Ulega alisema, kwa sasa mpango huo umeanza katika mikoa ya Tabora, Morogoro,

Arusha, Pwani na Mtwara.

Mikoa hiyo imechaguliwa kuanza mpango huo kwa kutumia vigezo mbalimbali kikiwemo cha Mkoa husika kuwa na mifugo mingi mfano Tabora ambao ndiyo unayoongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi nchini ambao ni zaidi ya milioni nne.

Mikoa mingine ya Arusha na Pwani imechaguliwa kuanza mpango huo kutokana kuwa na viwanda vingi hasa vya kuzalisha na kuchakata mifugo.

Mkoa wa Morogoro umechaguliwa kutokana na kuwa ugomvi wa kikabila kutokana kuwa na mifugo ambayo inasababisha ugomvi na wakulima kuhusu maeneo ya malisho, hivyo vijana

watatumia fursa hiyo ya kununua mifugo, kunenepesha na kuuza viwandani ili kupunguza uwingi wa mifugo.

Kwa upande wa mkoa wa Mtwara, umechaguliwa kutokana na kuwa karibu na nchi ya Comoro ambayo ni mnunuzi mkubwa wa ng'ombe nchini na kwenda kuchakata katika nchi yao.

Katika kupanua na kuimarisha mpango mkakati huo, wizara inakusudia kwenda katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwachukua vijana na kuwaingiza katika mpango huo wa kununua mifugo na kunenepesha na kuuza kwenye viwanda vya kuchakata nyama.